**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA KILOSA**

**SHULE YA SEKONDARI LUMBIJI S.L.P 334, KILOSA**

**FOMU YA MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE**

**KUMB. LSS/E1/001** **TAREHE**........................../..............................

MZAZI/MLEZI WA: ...............................................................................................

YAH: **KIDATO CHA** ......................................................................**MWAKA** ..........................................

Nakujulisha kuwa mwanao ......................................................namba..................

Amechaguliwa kujiunga na masomo ya sekondari katika shule ya sekondari Lumbiji.

Unatakiwa kumleta mwanao tarehe ....................................bila kukosa.

Shule ya sekondari Lumbiji ipo umbali wa kilometa 19 kasikazini wa barabara kuu Dumila –Kilosa.

**A. MALIPO MBALIMBALI**

- Hakuna malipo yoyote yanayohitajika kwani huu ni utekelezaji wa sera ya Elimu bila malipo.

**B. SARE ZA SHULE**

Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na sare mpya jozi mbili ili kumuweka nadhifu wakati wote .Sare hizi zitashonwa na mzazi/mlezi mwenyewe.

**i. WASICHANA**

- Sketi mbili (02) za kijana (iwe ndefu chini ya magoti)
- Shati mbili (02) nyeupe mikono mifupi
- Sketi ya bluu na fulana ya bluu moja (01) kwa ajili ya kazi za nje na michezo.
- Sweta la kijani moja(1) huvaliwa wakati wa baridi tu
- Viatu vyeusi vya ngozi vyenye gidamu jozi mbili (02) visigino vifupi
- Raba na soksi ndefu nyeupe kwa ajili ya michezo
- Soksi nyeupe jozi mbili (02) ziwe fupi

**ii. WAVULANA**

- Suruali mbili za kijani
- Mshati mawili (02) meupe mikono mifupi
- Suruali moja (01) ya bluu, bukta moja (01) ya bluu na fulana moja ya bluu kwa ajili ya kazi za nje na michezo.
- Sweta moja (01) la kijani ( huvaliwa wakati wa baridi tu)

- Viatu vya ngazi nyeusi vyenye gidamu na visigino vifupi jozi mbili (02)
- Raba na soksi ndefu nyeupe jozi moja (01) kwa ajili ya michezo

**C. MAHITAJI MENGINE**

- Daftari 20 au counter book 10
- Mkee wa vifaa vya hesabu ( mathematics set )
- Rula (01), pensel (01), mfutio (01) , kalamu ya wino wa bluu au nyeusi
- Kamusi 01 ya Kiswahili au kingereza

**NB**

Nasisitiza kwamba sare za shule ni zile zilizokubaliwa na shule rangi na mshono wake. Sare yoyote itakayoshonwa nje ya utaratibu wa shule haitambulika na kutumika shuleni.

Mwanafunzi lazima aje na barua hii siku ya kuripoti shuleni.

**"KARIBU SANA LUMBIJI SEKONDARI"**

______________________

**CHESCO .A. ANYIGULILE**
**MKUU WA SHULE**

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA KILOSA

SHULE YA SEKONDARI LUMBIJI

S.L.P 334, KILOSA

**SHERIA ZA SHULE**

Jumuiya ya shule ya sekondari Lumbiji ni kitu kimoja na tufikiri na kuwaza pamoja ili tutende yale ambayo yatailetea jamii yetu maendeleo ya kweli na kupafanya Lumbiji sekondari kuwa mahali pa kuendeza na kutamanika kuishi.

Motto wetu " Elimu kwa maisha bora" kwa hiyo Elimu itakuwa kwenye kichwa chenye nidhamu nzuri.

**A. HESHIMA**

i. Motto wa shule ni kuona kwamba

a. Wanafunzi wanapendana na kuheshimiana
b. Wanawaheshimu viongozi walioachagua
c. Matumizi ya lugha chafu, matusi, matukano na masengenyo pia kupigana ni marufuku popote pale mwanafunzi wawepo nje au ndani ya darasa au bweni.

**B. HESHIMA KWA WALIMU NA WAFANYAKAZI WASIO WALIMU**

a. Wanafunzi wanalazimika kusimama anapopita mwalimu, mfanyakazi asiye mwalimu pamoja na watu waliowazidi umri.Wanafunzi wanapaswa kusalimia kwa heshima wale wote waliowazidi umri.
b. Wanafunzi wanapaswa kuwaheshimu walimu na wafanyakazi wote bila ubaguzi.
c. Utani wowote ule kati ya waafunzi na walimu wa shule na wafanyakazi ni marufuku.
d. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuwa na uhusiano wa kimapenzi na mwalimu ( mfanyakazi ) wa shule au mtu yeyote.

**C. HESHIMA KWA JUMUIYA NJE YA SHULE**

a. Wanafunzi wanalazimika kuwaheshimu viongozi wote wa umma kwa ujumla.Wanatakiwa kujiweka tayari wakati wowote kujitolea kwa shughuli mbalimbali za ujenzi wa Taifa inapolazimika.
b. Wageni wote wanapofika shuleni wapokelewe kwa heshima na kupewa msaada wa kupelekwa kwa mwalimu wa zamu ambaye ataelewa ni wapi pa kumpeleka.

**D. HESHIMA KATIKA KAZI**

Uvivu, uzembe na utegaji katika kazi zingine uwe ni mwiko kwa kila mwanafunzi.

**E. HESHIMA KATIKA MALI**

a. Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa mwangalifu katika kila mali yake na wanafunzi wenzake.
b. Utunzaji wa mali ya Umma unapewa kipaumbele na ni sharti kila mwanafunzi atunze vifaa vyote vya shule kwa uangalifu.Uharibifu wa kitu chochote cha shule lazima uripotiwe kwa mwalimu wa zamu/darasa bila kuchelewa.

c. Uharibifu, upotevu na uvunjaji wa mali ya shule ni lazima aliyehusika alipe. Kama mali ya shule imeharibika au kupotezwa na kikundi bila kumtaja aliyehusika , basi kikundi chote kitawajibika kulipa mali hiyo.

d. Ni marufuku kuandika katikam vitabu vya shule , madawati, meza au kuta.

**F. HESHIMA KWA TAIFA**

Wanafunzi wanawajibika kuonyesha heshima ya juu na kuwa na nidhamu ya dhati kwa:-

a. Bendera ya Taifa
b. Nembo ya Taifa ( Courts of Arms)
c. Wimbo wa Taifa
d. Viongozi wa Taifa
e. Picha za viongozi wa Serikali

**I. USAFI**

a. Kila mwanafunzi lazima awe msafi wa mwili, akili na mawazo .Sare ya shule lazima iwe safi nyakati zote iwe inayoonyesha heshima.

1. **WAVULANA:** Nywele zikatwe na kuchanwa vizuri. Ni lazima ziweze kuhifadhi njiti ya kiberiti.Usinyoe"Punk" ,kipara au denge.Huruhusiwi kufuga ndevu.Huruhusiwi kuvaa nguo za nyumbani ukiwa shuleni hapa .Baada ya masomo unatakiwa kuvaa sare ya kazi.Huruhusiwi kuvaa suruali inayovuka kiuno kwenda chini.
2. **WASICHANA:** Ni marufuku kujipamba au kuvaa skirt fupi ( mini – skirt) ukiwa shuleni au upewapo ruhusu kwenda nje ya shule.Haruhusiwi kupaka wanja, rangi ya kucha , kuvaa bangili, herein, mkufu, kunyoa nyusi, kuweka nywele dawa ( curl, relaxer, steamer) kunyoa kihuni au kujichubua.

**II. USAFI WA TABIA**

1. Ni marufuku mwanafunzi kuvuta sigara, tumbaku, madawa ya kulevya, kunywa pombe au kujihusisha na wizi wa aina yeyote.
2. Ni marufuku kwa mwanafunzi kumtembelea mwalimu au mfanyakazi wa shule nyumbani kwake.
3. Ni marufuku mvulana na msichana kuingia kwenye nyumba ya kulala wageni au maeneo yaliyojificha wakati wakiwa shuleni au wakitoka shuleni.
4. Mvulana haruhusiwi kuingia hostel ya wasichana .Pia wasichana hawaruhusiwi kuingia kwenye hostel ya wavulana.
5. Urafiki wa kukaribishana nyumbani kati aya mvulana na msichana uepukwe kadri iwezekanavyo.
6. Hairuhusiwi kuwa na uhusiano wa mapenzi kati ya mwanafunzi msichana na mvulana au mtu yeyote.

**III. MIPAKA**

- Mwanafunzi ataonyeshwa mipaka ya shule
- Haruhusiwi kutoka nje ya mipaka ya shule bila kibali cha Mkuu wa shule au Makamu wake.
- Haruhusiwi kuingia Ofisi ya Mkuu wa shule , Ofisi ya Makamu wa Mkuu wa shule , chumba cha walimu (Staff room), Ofisi za wakuu wa Idara zote, Maabara , jikoni, nyumba za walimuau wafanyakazi wasio walimu isipokuwa kwa kibali cha Mkuu wa shule au Makamu wake au Ofisa mhusika na Ofisi hiyo.

**IV. MAHUDHURIO NA KUWAHI SHULENI**

1. Ni lazima kila mwanafunzi awahi shuleni na kutimiza wajibu wake.Roll Call ni saa 1:00 asubuhi kwa wanafunzi.
2. Kila mwanafunzi asikose shule.Kama kunatatizo la ugonjwa taarifa itolewe kesho yake pamoja na cheti cha Daktari ikiwa ni sababu nyingine kama msiba taarifa iletwe shuleni.Kama mwanafunzi amefiwa na ndugu , jamaa akiwa shuleni taarifa itolewe kwa Mkuu wa shule au makamu wake kama Mkuu hayupo , na si kwa mwanafunzi mhusika.
3. Ruksa ya kutokuwa shuleni itatolewa na Mkuu wa shule ua Makamu wa shule wake endapo Mkuu wa shule hatokuwepo.
4. Mwanafunzi haruhusiwi kuondoka eneo la shule ( kutoka nje ya mipaka ya shule) bila ruhusa ya Mkuu wa shule au mwalimu wa zamu kwa waendao kwenye matibabu.
5. Kila mwanafunzi wa hostel awepo bwenini kwake baada ya maandalizi ya usiku (Preparations) kwisha.

## V. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

1. Wizi
2. Uasherati, ubakaji, ushoga
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya
4. Uvutaji wa bangi
5. Makosa ya jinai
6. Kupigana au kupiga
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma
8. Kudharau bendera ya Taifa
9. Kuoa au kuolewa
10. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule
11. Kutoa mimba
12. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuharibu amani na usalama wa watu
13. Kukataa adhabu kwa makusudi.